

# MAJIBU YENYE FAIDA

NO.9

KUHUSU

MASWALI YA MIFUMO MIPYA

MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAWZA AL FAWZAN

MFASIRI : ABUL 'AALIYAH UMAR BIN MUHAMMAD KONDO

PONGWE - TANGA - TANZANIA

## Swali la kumi na moja:

Jamaat-ut-Tablighi, kwa njia ya kupiga mfano wanasema. Sisi tunataka kupita juu ya njia ya Ahlu-s-sunna waljama'ah, lakini baadhi yao huwenda wanakosea na wanasema: vipi mnatuhukumu mnawatahadharisha watu na sisi?

**Jawabu:** Jamaat-ut-Tablighi (kundi la Tablighi) wameandika kuhusu wao wale waliotoka pamoja nao na wakawasomesha na wakaandika kutoka kwao mengi na wakayagudua makosa ambayo wako nayo, basi lazimianeni kusoma yale yaliyo andikwa kuhusu wao ili ibainike kwenu hukmu katika hili.

Alhamdulillah Allah ametutosheleza kuepukana na kumfuata Fulani na Fulani, sisi tunayo njia ya Ahlu-s-sunna waljama'ah tunalazimiana nayo, na si wajibu juu

yetu kulazimiana na kundi la Tablighi au (kundi jingine) lisilokuwa tablighi, hatuna haja nalo, basi hakuna baada ya haki ila upotevu.

Ama uhakika wao, kwa hakika vimeandikwa kuhusu wao vitabu vingi, vichungulieni (vipitieni) mtajua (Tablighi) na (mtawajua) wale ambao waliyoandika kuhusu wao miongoni mwa waliyotoka pamoja nao na wakasafiri nao na wakachanganyika nao na wakaandika kuhusu wao kwa maarifa na kwa ubainifu.

### **Swali la kumi na mbili:**

Je..! haya makundi (yanayojinasibisha kwenye uislamu) yanaingia katika makundi sabini na mbili yaliyo angamia (ya motoni)?

**Jawabu:** Ndiyo, kila anaewakhalifu Ahlu-s-sunna waljama'ah katika wale ambao wanajinasibisha kwenye

uislamu katika Da'wah, au 'Aqidah, au katika chochote katika misingi ya Imani basi hakika huyo anaingia katika makundi sabini na mbili, na inamuenea yeye ahadi ya moto, na atakuwa anastahiki (kusemwa vibaya) kulauamiwa na kuadhibiwa kwa kiasi cha kukhalifu kwake.